HAKIARDHI

LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

# MADAI YA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI NA RASILIMALI NYINGINEZO





# MADAI YA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI NA RASILIMALI NYINGINEZO

IMEANDALIWA NA
HAKIARDHI



**Mchapishaji:** HAKIARDHI

**Mchapaji**: iPrint Ltd

**Msanifu** Bakari Kacheuka

© HAKIARDHI 2020

Kitabu hiki kimechapishwa kwa hisani ya Rosa Luxembourg Stiftung (RLS) inayofadhiliwa na Wizara ya Ushirikiano wa Kiuchumi na Maendeleo ya Kijerumani.

# YALIYOMO


**SEHEMU YA KWANZA ....................................................................1**

1.0 UTANGULIZI ........................................................................................ 1

1.1 TAFSIRI NA VIGEZO VYA WAZALISHAJI WADOGO ....................................... 1

1.2 MUKTADHA NA MCHANGO WA WAZALISHAJI WADOGO NCHINI .............. 1

1.3 CHANGAMOTO ZA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI ....................... 4

1.4 HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2015 – 2020) ........................................................................ 6

**SEHEMU YA PILI ........................................................................9**

2.0 MADAI YA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI NA RASILIMALI NYINGINEZO .............................................................................. 9

2.1 UTAWALA NA USIMAMIZI WA ARDHI ............................................. 9

2.2 MFUMO WA KUMILIKI ARDHI NCHINI ............................................ 11

2.3 HAKI ZA WANAWAKE NA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA ARDHI ........... 12

2.4 UKUAJI WA MIJI ........................................................................ 15

2.5 UKUAJI WA VIJIJI ..................................................................... 17

2.6 UPIMAJI WA ARDHI ................................................................... 19

2.7 MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI YA VIJIJI .................................. 20

2.8 UWEKEZAJI KATIKA ARDHI ......................................................... 22

2.9 MFUMO WA TAARIFA ZA ARDHI .................................................... 25

2.10 MFUMO WA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI ........................... 27

2.11 TATHMINI NA UFUATILIAJI WA MASUALA YA ARDHI ....................... 29

**HITIMISHO ........................................................................28**

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 TAFSIRI NA VIGEZO VYA WAZALISHAJI WADOGO

Wazalishaji wadogo wanatafsiriwa kuwa ni wale ambao hawategemei nguvu kazi ya ajira ya kudumu au rasmi badala yake uzalishaji mali wao hutegemea nguvu kazi ya familia na zana za asili. Kuna makundi mbalimbali ya wazalishaji wadogo hapa nchini ambayo kwa kiasi kikubwa yanategemea kilimo, ufugaji, uvuvi, kuokota matunda na uchimbaji mdogo wa madini katika kuendesha maisha yao kila siku. Makundi haya ni pamoja na: ***wakulima wadogo, wafugaji wadogo, wachimbaji wa madini wadogo, wavuvi wadogo, waokota matunda na warina asali.***

### 1.2 MUKTADHA NA MCHANGO WA WAZALISHAJI WADOGO NCHINI

Ardhi ni mojawapo ya rasilimali muhimu kwa uhai wa binadamu na viumbe vyote. Ardhi hubeba rasilimali nyingine zote za asili na miundo mbinu. Vilevile, ardhi huchangia katika ukuaji wa maendeleo ya mtu mmoja mmoja, jamii kwa ujumla na uchumi wa Taifa. Makundi ya wazalishaji wadogo yanategemea ardhi katika shughuli mbalimbali za kilimo, uvuvi, ufugaji, uchimbaji wa madini na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Mfano, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wote ni wazalishaji wadogo wanaotegemea ardhi katika shughuli zao za uzalishaji mali.

Umuhimu wa ardhi kwa makundi haya, si tu unatanabaishwa kwenye sera na sheria, bali umeainishwa kwenye mikakati na programu za maendeleo ya nchi. Mfano, moja ya malengo ya Sera ya Ardhi ya 1995, ni kuhakikisha kuwa kuna ugawaji na upatikanaji sawa wa ardhi kwa wananchi wote. Hii ina maana kuwa ugawaji na

upatikanaji wa ardhi lazima uzingatie haki za makundi yote nchini, ikiwemo makundi haya ya wazalishaji wadogo hasa wanawake.[1] Vile vile sera inasema kuwa haki za kimila za wazalishaji wadogo, yaani wakulima wadogo na wafugaji, ambao ni wengi nchini, zitambuliwe, ziainishwe, na kulindwa kisheria.[2]

Sera ya Mifugo ya mwaka 2006, inaainisha kuwa serikali itaweka utaratibu wa kuibua mifumo bora ya uzalishaji itakayoongeza tija miongoni mwa wafugaji wadogo.[3] Kwa upande mwingine, Sheria za Ardhi, yaani sheria namba. 4 na 5 za mwaka 1999, zote kwa pamoja zinatambua mfumo wa umiliki wa ardhi kimila. Mfumo huu unalenga kutambua haki na maslahi ya wazalisha wadogo wanaopata, kutumia na kumiliki ardhi kwa njia ya kimila. Vilevile, programu ya Kuendeleza Kilimo ya Awamu ya Pili (ASPD II), inalenga kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo (kilimo, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, usalama wa chakula na lishe.[4]

Kwa kiasi kikubwa wazalishaji wadogo ndio wachangiaji wakubwa katika ukuaji wa pato la Taifa na kukuza uchumi wa nchi. Kwa mfano, sekta ya kilimo inachangia zaidi ya asilimia 40 ya pato la Taifa na wakulima wadogo ndio wawekezaji wakubwa katika sekta ya kilimo ambapo wanazalisha takribani asilimia 75 ya chakula chote kinachozalishwa nchini. Uzalishaji wa mazao ya bustani hususan mboga, matunda na viungo huchangiwa kwa asilimia 85 na sekta isiyo rasmi ambayo wakulima wadogo ndio wanaozalisha na kuuza mazao hayo katika masoko ya ndani.[5]

1 Sehemu ya 2.1 ya Sera ya Taifa ya Ardhi, 1995
2 Sehemu 2.2. ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995
3 Sehemu ya Dibaji ya Sera ya Mifugo ya Mwaka 2006
4 Sehemu ya 7 ya ASDP II, 2017
5 Hotuba ya Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga (Mb), kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka 2020/2021, Uk. 17

Wafugaji wa asili wanachangia kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji wa nyama, maziwa, ngozi na mbolea. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka 10, kuanzia mwaka 1995 mpaka mwaka 2005, ufugaji wa asili ulichangia uzalishaji wa tani 134,500 za nyama. Hivyo uzalishaji wa nyama kwa kipindi hicho uliongezeka kutoka tani 244,000 hadi tani 378,500 sawa na ongezeko la asilimia 55 ambapo sehemu kubwa ilitokana na ufugaji wa asili. Pia, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita milioni 555 hadi bilioni 1.38 ambapo asilimia 70 ilichangiwa na sekta ya ufugaji wa asili. Vilevile, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka mayai milioni 380 hadi bilioni 1.8. asilimia kubwa ikiwa imechangiwa na wafugaji wa asili.[6]

Wachimbaji wadogo wa madini, wanachangia kiasi kikubwa katika kuongezeka pato la Taifa. Mfano, kwa kipindi cha kuanzia Machi 2019 hadi Februari 2020, kupitia masoko ya madini nchini, wachimbaji wadogo wamefanya biashara ya madini yenye thamani zaidi ya shilingi trilioni moja na wameiingizia Serikali mapato kwa kulipa mrabaha na ada ya ukaguzi wa zaidi ya shilingi bilioni sabini na nane. Vilevile, wachimbaji wadogo wanachangia karibu asilimia 0.3 ya mapato yao kwenda Halmashauri za wilaya na hivyo kuongeza kipato katika serikali za mitaa.[7]

Wanawake nao ni mojawapo ya kundi la wazalishaji wadogo lenye mchango mkubwa katika ujenzi wa jamii na kukuza uchumi wa Taifa. Inakadiriwa kuwa takribani asilimia 52 ya idadi ya watu wote nchini ni wanawake. Pia wanawake wanashiriki katika uzalishaji mali kwa takribani asilimia 60 hadi 80 ya chakula kinachotegemewa katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara. Tafiti nyingi zinaonyesha kuwa asilimia 20 tu ya wanawake ndio wanaomiliki ardhi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hali hii inachangia wanawake kuendelea kuwa masikini, kunyanyaswa na kudhalilishwa.

6 Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo
7 Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Madini, 2020/2021

## 1.3 CHANGAMOTO ZA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI

Pamoja na mchango mkubwa wa wazalishaji wadogo katika uchumi wa nchi, bado wanaendelea kukumbana na changamoto mbalimbali zinazohusisha ukosefu wa masoko ya uhakika, pembejeo za kutosha na za wakati, mapungufu katika mifumo ya kisera na kisheria inayokumbatia wazalishaji wakubwa na wawekezaji kutoka nje kuliko makundi haya ya wazalishaji wadogo. Vilevile, wakulima wadogo wanakosa ruzuku na pembejeo za kilimo, pamoja na ukosefu wa ulinzi wa uhakika wa ardhi kwa ajili ya uzalishaji. Ukiachana na changamoto hizi za jumla, sehemu hii inaangazia changamoto za wazalishaji wadogo zenye mguso wa moja kwa moja na upatikanaji, matumizi na usimamizi wa ardhi kama inavyoainishwa hapa chini:

**Moja** ni kukosekana kwa mifumo imara inayolinda haki na maslahi mapana ya wazalishaji wadogo katika ardhi. Mfano, mfumo wa umilikaji wa ardhi, changamoto za upatikanaji wa rasilimali za maji na malisho zinazoathiri wazalishaji wadogo. Hii ni pamoja na kasi ndogo ya kutenga na kumilikisha ardhi kulingana na taratibu za kisheria au kimila.

**Mbili** ni kupanuka kwa shughuli za kilimo, hasa kilimo biashara, katika maeneo yaliyokuwa yanatumika kwa kufuga na kuchungia mifugo.

**Tatu** ni kasi ya kuhuisha na kupanuliwa kwa maeneo ya hifadhi za wanyamapori kama hifadhi za taifa, mapori tengefu, mapori ya akiba, na maeneo ya hifadhi za jamii ambayo kwa pamoja yanazuia kuendelezwa kwa maeneo ya wakulima na wafugaji.[8] Hii imesababisha hifadhi za wanyamapori kuwa karibu na wananchi na hivyo kusababisha migogoro ya wanyama na binadamu hasa pale wanyama wanapoingia kwenye mashamba ya wananchi na kula mazao au mifugo yao.

8 Sehemu ya 1.3 ya Sera ya Kilimo ya Mwaka 2006

**Nne** ni ushirikishwaji hafifu wa wazalishaji wadogo katika kutoa maamuzi ya upangaji wa matumizi na usimamizi wa ardhi yao. Mfano, pamoja na ukweli kuwa wafugaji wa asili ni kundi kubwa la wazalishaji wadogo, lakini wamekuwa hawashirikishwi kikamilifu katika mchakato wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji. Hivyo kusababisha maeneo mengi yanayofaa kwa ufugaji kutengewa matumizi mengine*.* Vilevile, baadhi ya maeneo ya mashamba ya wakulima wadogo yamekuwa yakiainishwa na kutengwa kama maeneo ya mipango miji bila kushirikisha wakulima wenyewe na bila kufanya utafiti wa kina juu ya madhara ya kutangaza mashamba hayo kuwa maeneo ya mipango miji. Hii imesababisha wakulima wadogo kushindwa kuendeleza shughuli za kilimo na kubaki kwenye sintofahamu ya hatma ya maisha yao.[9]

**Tano** ni haki za wanawake katika kupata, kutumia, kumiliki na kufanya maamuzi juu ya ardhi hazizingatiwi ikilinganishwa na wanaume. Hii ni kutokana na mila na desturi zinazowanyima wanawake njia halali za kumiliki ardhi ikiwemo kurithi ardhi za wazazi na wenza wao na hivyo kutoshiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Wanawake wanapewa fursa ya kutumia ardhi na kufanya shughuli za uzalishaji lakini wanaume ndio wanaoamua namna ya kutumia mapato yanayotakana na nguvu ya mwanamke.

**Sita** ni ubidhaishaji wa huduma za kijamii kama vile afya, elimu, maji na pembejeo za kilimo, hii imepelekea changamoto kubwa kwa wazalishaji wadogo ambapo hufikia hatua wanauza chakula cha akiba ili wamudu gharama za huduma hizi muhimu.

**Saba** ni ushirikishwaji hafifu wa wazalishaji wadogo katika michakato ya utungaji na mabadiliko ya sera na sheria za ardhi na rasilimali nyinginezo, hivyo kupelekea sera na sheria husika kutoakisi maoni na mahitaji ya wazalishaji wadogo.

9 Uzoefu kutokana na mradi wa Urasimishaji Ardhi wilaya za Kilombero, Malinyi na Ulanga, 2016-2019

## 1.4 HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2015 – 2020)

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, serikali imechukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuimarisha utawala na usimamizi wa ardhi nchini na hivyo kuwezesha wazalishaji wadogo kutekeleza shughuli zao. Kwa ujumla hatua hizi ni pamoja na kufuta hati za mashamba makubwa yasiyoendelezwa kwa muda mrefu, kuchukua hatua mbalimbali za kutatua migogoro ya ardhi, kutunga na kuboresha sheria na sera kwa lengo la kuimarisha usimamizi na umiliki wa ardhi. Mahususi kabisa, serikali imechukua hatua zifuatazo:

**Kwanza** ni ufutaji wa hati za mashamba ya uwekezaji ambayo yalikuwa hayajaendelezwa kwa muda mrefu katika maeneo mbalimbali nchini. Mfano, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, alifuta jumla ya hati 14 za mashamba yaliyoshindwa kuendelezwa katika Wilaya za Kilosa, Mvomero na Kilombero.[10] Vilevile, Mh. Rais alifuta hati ya shamba la mkonge la Kibaranga, wilaya ya Muheza lenye ukubwa wa hekta 5,730.[11] Mashamba mengine yalipunguzwa ukubwa kama vile shamba la Kampuni ya KPL Kilombero lilipunguzwa hekta 810 na shamba la Kapunga Mbarali hekta 4,620.[12]

Pamoja na ufutaji wa hati hizi lakini bado kuna changamoto ya wazalishaji wadogo kutokurudishiwa mashamba hayo kama alivyoagiza Mhe. Rais. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro wakulima na wafugaji wameendelea kudai kurudishiwa mashamba hayo kwa usawa.

**Pili** ni jitihada za kutatua migogoro ya ardhi, hasa ile ya wananchi na maeneo ya hifadhi, mwaka 2019, Rais aliunda Kamati ya Mawaziri kubainisha vijiji vyote vilivyoainishwa kuwa katika hifadhi

10 Taarifa ya EAT ya tarehe 14 August, 2017
11 Mtanzania digital June 7, 2016
12 Bajeti ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2016/17

za wanyamapori. Kufuatia mapendekezo ya Kamati, Baraza la Mawaziri mnamo mwezi Septemba 2019, liliridhia kuwa vijiji 920 kati ya vijiji 975 vilivyokuwemo ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na ranchi kuhalalishwa rasmi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na kijamii. Aidha, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya vijiji 55 vilivyobaki ili kutoa maamuzi. Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta na wadau mbalimbali inaendelea kuhakiki mipaka ya vijiji husika, kupanga na kupima ili kuzipa Serikali za vijiji mamlaka ya kusimamia ardhi za vijiji hivyo.[13]

**Tatu** ni serikali kuanzisha na kutekeleza miradi mbalimbali ya mipango ya upimaji wa mashamba na viwanja kwenye ardhi za mijini na vijijini. Miradi ya urasimishaji wa ardhi ambayo imekuwa ikifanywa na serikali yenyewe pamoja na makampuni binafsi ya upimaji wa ardhi. Vilevile kumekuwepo na miradi mikubwa ya mipango ya matumizi ya ardhi na utoaji wa vyeti vya Hakimiliki za kimila katika wilaya za Ulanga, Malinyi na Kilombero pamoja na miradi mingine katika wilaya nyinginezo nchini. Changamoto kubwa katika miradi ya upimaji wa ardhi imekuwa ni ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya Hati za Hakimiliki za Kimila. Kuna dhana iliyojengeka kuwa Hati ya Hakimiliki ya kimila ni kwa ajili ya kuchukulia mikopo benki. Dhana hii ni matokeo ya ukosefu wa elimu na inaweza kuhatarisha uhakika na usalama wa kumiliki ardhi za wazalishaji wadogo pale watakaposhindwa kurejesha mikopo waliyochukua.

**Nne** ni serikali kuanzisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Kilimo ya mwaka 2013. Sheria na Sera hizi zilikuwa na malengo ya kuboresha usimamizi na utawala wa ardhi, na kutenga maeneo mahususi kama ardhi ya kilimo. Hata hivyo, michakato ya utungaji wa sheria na uandaaji wa sera ilifanyika kwa ukimya bila kushirikisha makundi makubwa ya wazalishaji wadogo.

13 Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya Mwaka 2020/2021, Ukurasa wa 48

**Tano** ni kutengwa kwa bajeti ndogo ya sekta ya ardhi kwa kuzingatia ukweli kuwa sekta ya ardhi sio kipaumbele katika vipaumbele mahususi vya serikali. Kwa mfano, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, sekta ya ardhi haikupewa kipaumbele cha bajeti ya kutosha. Mafanikio ya sekta nyingine muhimu kama vile afya, elimu, kilimo, maliasili na utalii, viwanda, miundombinu, ujenzi, nishati na madini hutegemea jinsi ardhi ilivyopangwa na kuratibiwa. Kutokana na umuhimu huo ni vyema Bajeti ya Wizara ya Ardhi ikapewa kipaumbele katika sekta tano za juu zinazotengewa bajeti ya kutosha ili kuwezesha maendeleo ya sekta nyingine.

Pamoja na ufinyu wa bajeti katika sekta ya ardhi, pamekuwepo na changamoto nyingine zinazowaathiri wazalishaji wadogo. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja kuongezeka kwa migogoro ya ardhi inayosababishwa na matumizi mbalimbali ya ardhi, mabadiliko ya tabianchi, migogoro ya mipaka ya vijiji na vijiji, kupanuka kwa miji, kuongezeka kwa ardhi za uwekezaji na hifadhi za wanyamapori, kukosekana kwa mipango thabiti na ya kutosha ya matumizi ya ardhi.

Kwa muda mrefu wazalishaji wadogo wamekuwa na madai mbalimbali ambayo yanapaswa kupewa kipaumbele na serikali ili kuhakikisha kuwa ardhi na rasilimali nyingine zinatumika kuwanufaisha wao kijamii na kiuchumi. Madai haya yamegawanywa katika makundi tisa kama ilivyoainishwa katika sehemu ya pili.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 MADAI YA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI NA RASILIMALI NYINGINEZO

### 2.1 UTAWALA NA USIMAMIZI WA ARDHI

**Muktadha:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ndio yenye dhamana ya kuhakikisha kuwa ardhi yote nchini inapangwa, inapimwa na kumilikishwa, hii ni katika kuhakikisha kuwa kuna uboreshwaji wa huduma mbalimbali hasa katika nyanja za uwekezaji katika ardhi, makazi na milki. Katika kuhakikisha huduma zinaboreshwa Wizara hapo awali ilianzisha ofisi za ardhi katika kanda tisa, pamoja na jitihada hizi bado kumekuwepo na vikwazo na changamoto mbalimbali, ni katika muktadha huu Wizara imeamua kuanzisha ofisi za ardhi kwa kuwateua makamishina wasaidizi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kwa takribani miaka mitano iliyopita kumekuwapo na jitihada za kurejesha ardhi zilizotwaliwa kwa ajili ya uwekezaji kwa wananchi ama wazalishaji wadogo, na pia ardhi zilizotengwa kwa minajili ya uhifadhi kurejeshwa kwa wanavijiji hasa pale ambapo kumekuwapo na migogoro ya kimatumizi.

**Changamoto:** Sheria za ardhi zinampa Kamishna wa Ardhi kuwa na mamlaka ya ushauri kwenye Halmashauri za Vijiji na wanavijiji juu ya usimamizi wa ardhi ya kijiji. Kumekuwepo na matumizi mabaya ya mamlaka hiyo hasa pale ushauri unaotoka kwa Kamishna kuchukuliwa kama ni uamuzi wa mwisho hivyo kuchukua nafasi ya maamuzi ya wanakijiji kuhusu ardhi yao. Wakati mwingine wanavijiji wamekuwa wakikosa ushauri wanaohitaji kutoka kwa Kamishna na pale unapopatikana basi unatolewa kwa lengo la kufanikisha maombi ya ardhi yanayohusisha uhawilishaji kutoka ardhi ya Kijiji kuwa ya Jumla kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

Utaratibu ulioainishwa kisheria wa ardhi ya kijiji kusimamiwa na Serikali ya kijiji na maamuzi ya mwisho kufanywa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Utaratibu huu umefanya kazi vizuri hasa katika maeneo ambayo wanakijiji wana uelewa mzuri wa haki zao za kisheria na taratibu za ardhi. Changamoto kuu ni kwamba elimu juu ya haki za ardhi na nafasi ya vyombo kama Mkutano Mkuu wa Kijiji haijawafikia wanavijiji walio wengi na pia hili ni suala endelevu, kwani kila mwaka wanapatikana wanavijiji wapya kwa maana ya kigezo cha kutimiza umri wa miaka 18 ili kukidhi takwa mojawapo ya kuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Kijiji.

### Mapendekezo:

- Halmashauri za vijiji na Mikutano Mikuu ya vijiji viendelee kuwa na dhamana juu ya ardhi ya kijiji hususani katika usimamizi, matumizi na ugawaji.
- Mkutano Mkuu wa kijiji uendelee kuwa ndio chombo chenye mamlaka ya juu (Milki ya hatma) katika maamuzi juu ya ardhi ya kijiji na wananchi wapewe elimu zaidi juu ya mamlaka yao hii.
- Halmashauri za vijiji zijengewe uwezo wa kusimamia ardhi na maliasili zilizopo ndani ya vijiji kwa niaba ya wanakijiji wote.
- Ugatuaji uliofanyika wa kuwateua Makamishina wasaidizi katika ngazi ya mikoa bila shaka utasaidia zaidi kufikisha huduma za kiushauri hadi ngazi ya kijiji kwa ufanisi zaidi.
- Ardhi zote ambazo zimetelekezwa na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi zirejeshwe kwa wazalishaji wadogo hususani wakulima, wafugaji na makundi mengineyo ya wazalishaji wadogo. Katika hili haki ya wanawake kumiliki ardhi izingatiwe
- Elimu juu ya sera na sheria zinazosimamia ardhi ijumuishwe katika mitaala ya elimu ya msingi, sekondari pamoja na vyuo ili kuwawezesha vijana kuwa na uelewa juu ya masuala yanayohusu haki za ardhi.

## 2.2 MFUMO WA KUMILIKI ARDHI NCHINI

**Muktadha:** Sera ya Taifa ya Ardhi 1995 pamoja na Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 zinatambua aina mbili za umiliki wa ardhi nchini ambazo ni umiliki wa ardhi kwa Hati na umiliki wa ardhi Kimila. Hati hutolewa kwa mmiliki wa ardhi katika kundi la ardhi ya jumla wakati umiliki wa kimila ambao umetengenezewa cheti cha hakimiliki ya kimila hutolewa kwa mmiliki wa ardhi ndani ya Kijiji.

Sheria za Ardhi zimeweka usawa katika aina hizo mbili za umiliki na tofauti ya msingi iliyopo ni kuwa hati itatolewa kwa ukomo wa muda maalum, yaani miaka 33, 66 au 99 wakati umiliki wa ardhi kimila hutolewa bila ukomo wa muda. Vilevile, mmiliki wa ardhi kwa hati anakuwa na hadhi ya mpangaji kwa kuwajibika kulipa kodi ya ardhi kwa Kamishna wa Ardhi kila mwaka wakati mmiliki wa ardhi kimila hana tozo ya kodi ya ardhi isipokuwa kama kijiji kimejiwekea utaratibu wa kutoza kodi hiyo.

**Changamoto:** Mfumo wa umiliki wa ardhi unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile kukosekana kwa uhakika wa umiliki pale ardhi inapohitajika kwa manufaa ya umma. Sheria ya Utwaaji namba 47 ya mwaka 1967 inampa Rais mamlaka ya kuchukua ardhi yoyote kwa manufaa ya umma ambapo sheria hiyo wakati mwingine imekuwa ikitumiwa vibaya na mamlaka za serikali kwa kuchukua ardhi za wananchi kwa kisingizio cha maslahi ya umma.

Vilevile, mfumo wa umiliki wa ardhi kimila umeshindwa kuakisi uhalisia wa umiliki kimila ambapo ardhi inamilikiwa kwa misingi ya koo husika kwa kuwa cheti cha hakimiliki ya kimila kinachotolewa ni lazima kiandikwe kwa jina la mtu. Hii imepelekea kuleta migongano kwenye koo ambazo bado zinahitaji kumiliki maeneo hayo kimila kwa kuwa wanapotaka kupima na kupatiwa hati ya kimila wanapaswa kukubali ardhi hiyo igawanywe kwanza ndio upimaji ufanyike kwa kipande cha mtu mmoja mmoja.

**Mapendekezo:**

- Mfumo wa umiliki ardhi kimila ufanyiwe marekebisho ili kuweza kuakisi uhalisia wa umiliki ardhi kimila.
- Utwaaji wowote wa ardhi sharti uzingatie ridhaa huru na fidia ya haki na kwa wakati itakayomuweka muathirika katika nafasi nzuri zaidi ya aliyokuwa nayo mwanzo.
- Ukomo wa ukubwa wa umiliki wa ardhi ndani ya vijiji uwe ni Ekari 100, hii inazingatia mahitaji ya ardhi ndani ya kijiji na kuondoa uwezekano wa kuhodhiwa ardhi kubwa na kikundi kidogo cha watu.
- Endapo mtu anamiliki ardhi zaidi ya kijiji kimoja ukomo wake utahesabiwa kwa kujumlisha ukubwa wa ardhi zote anazomiliki. Ikiwa mmiliki anahitaji eneo zaidi ya ekari 100 basi mtu huyo aombe ardhi kwenye kundi la ardhi ya jumla.

## 2.3 HAKI ZA WANAWAKE NA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA ARDHI

**Muktadha:** Katiba ya nchi na sheria za ardhi zinatambua haki za wanawake katika ardhi kwa maana ya kupata, kutumia, kumiliki na kudhibiti ardhi, bado wanawake wameendelea kupata changamoto ili kuzifikia haki hizo[14]. Hata hivyo kwa miaka ya karibuni kuna mabadiliko chanya katika jamii ambayo imeanza kutambua kuwa mwanamke anayo haki sawa na mwanaume katika umiliki wa ardhi. Mabadiliko hayo yamechangiwa hasa na jitihada mbalimbali za serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kupitia mafunzo na kampeni mbalimbali zinazolenga kuhakikisha haki za wanawake katika ardhi zinatambulika na kulindwa[15].

14 Kifungu cha 3(2) cha Sheria za Ardhi namba 4 na 5 (1999)
15 Kampeni ya Linda ardhi ya mwanamke (2019-2030)

Haki za kumiliki mali kwa wanawake zinaboresha usawa wa kijinsia ambao unapelekea maendeleo. Hivyo haki ya kumiliki mali kwa wanawake ni muhimu kwani ndiyo inayompa mwanamke ulinzi wa kiuchumi, hadhi ya kijamii na kisheria na hivyo kuweza kuendelea kiuchumi. Ikumbukwe kuwa, wanawake wanachangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa hususani walio katika sekta isiyo rasmi kama vile kilimo. Mpaka kufikia mwaka 2014, wanawake waishio vijijini walikuwa wanashiriki katika kilimo kwa asilimia 90.[16]

**Changamoto:** Uwepo wa mila, desturi na dini kandamizi ni tatizo kubwa katika umiliki wa ardhi kwa wanawake. Mila na desturi za jamii nyingi zimekuwa zikimnyima mwanamke haki ya kumiliki na kufanya maamuzi juu ya ardhi ya familia au ukoo. Mwanamke amekuwa akionekana ni mtu asiyestahili kumiliki ardhi kwa fikra kwamba akiolewa atakwenda kumiliki ardhi kwa mumewe. Vilevile watoto wa kike hawarithi ardhi za wazazi wao kwa usawa kama walivyo watoto wa kiume.

Kukosekana usawa wa kijinsia, hususani chini ya mifumo ya kimila, inachangia sana kunyima haki za wanawake katika ushiriki wa maamuzi kuhusu ardhi na rasilimali na umiliki wa ardhi ingawa ndio wazalishaji mali wakubwa hali inayowafanya kutonufaika na matunda ya kazi yao.[17]

Udhaifu wa kimaamuzi katika vyombo vya usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi katika ngazi za vijiji na kata ni changamoto katika upatikanaji wa haki za ardhi kwa wanawake. Kukosekana kwa vitendea kazi na weledi miongoni mwa wajumbe wa vyombo hivi unapelekea haki za wanawake kucheleweshwa au kutopatikana kabisa[18].

16 Ripoti ya Shirika la Chakula duniani kwa Tanzania (2014)
17 Ripoti ya Tume ya Rais juu ya masuala ya Ardhi (1992)
18 Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (2017)

Uzoefu unaonyesha kuwa ushiriki wa wanawake katika vyombo vya usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa sio mzuri. Mfano idadi ya wajumbe wanawake kwenye Mabaraza ya Ardhi ya vijiji, Mabaraza ya Kata na Halmashauri za vijiji imeendelea kuwa pungufu.

### Mapendekezo:

- Wazalishaji wadogo wanahitaji mambo yafuatayo yatekelezwe ili kuhakikisha kuwa wanawake wanapata haki zao za msingi kama ambavyo Katiba na sheria za nchi zinaelekeza;
- Vyombo vya usimamizi wa ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi kama vile Mabaraza ya Ardhi ya vijiji, Mabaraza ya Kata na Halmashauri za vijiji vijengewe uwezo ili kutekeleza majukumu yao kwa usahihi ikiwa ni pamoja na kuzingatia na kutunza haki za ardhi za wanawake na watu wenye ulemavu.
- Serikali ielekeze nguvu kubwa katika kukuza uelewa wa jamii juu ya sheria za ardhi na haki za ardhi kwa wanawake na watu wenye ulemavu.
- Kuwepo na usimamizi thabiti wa serikali juu ya utekelezaji wa sheria za ardhi ili kukabiliana na mila na desturi kandamizi dhidi ya wanawake na watu wenye ulemavu.

## 2.4 UKUAJI WA MIJI

**Muktadha:** Katika kipindi cha takribani muongo mmoja uliopita, Tanzania imeshuhudia kasi kubwa ya ukuaji wa miji, kiwango cha ongezeko la watu katika miji mingi nchini kimeendelea kuwa kikubwa kila mwaka. Uhamiaji wa watu kutoka vijijini kwenda mijini kumepelekea kupanuka kwa maeneo ya miji. Pia idadi ya miji inaongezeka kadri vijiji vinavyopanuka na kubadilika kuwa miji. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 1967 wakazi wa miji walikuwa asilimia 5.7 na mwaka 2012 iliongezeka kufikia asilimia 29.1. Ukuaji wa miji nchini una kasi ya asilimia 7 – 11 kwa mwaka kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.5 kwa Afrika.[19]

Eneo linapokuwa tayari kuendelezwa kimji, hupangwa na kupimwa kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007 ambayo imeainisha taratibu za upangaji na uendelezaji wa maeneo mapya ya miji ambazo ni;

**Hatua ya kwanza** ni eneo kutangazwa kama ni eneo la mpango linalotakiwa kuendelezwa kimji;

**Hatua ya pili** ni uhamasishaji wa wadau mbalimbali;

**Hatua ya tatu** ni ukusanyaji wa takwimu na taarifa mbalimbali;

**Hatua ya nne** ni uchambuzi wa takwimu na taarifa mbalimbali;

**Hatua ya tano** ni kutayarisha misingi ya mpango wa jumla;

**Hatua ya sita** ni kutayarisha mpango wa awali;

**Hatua ya saba** ni wadau kupitia na kuthibitisha mpango wa awali;

**Hatua ya nane** ni kurekebisha mpango wa awali uliopitishwa na mkutano wa wadau;

19 Tamko la Waziri wa nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI Mhe. Seleman S. Jaffo katika kuadhimisha ya siku ya miji duniani, 31 Oktoba, 2018.

**Hatua ya tisa** ni kuthibitishwa kwa mpango;

**Hatua ya kumi** ni kufanyika kwa uthamini wa mali za wananchi, na ulipaji wa fidia kwa nia ya kutwaa eneo la mpango;

**Hatua ya kumi na moja** ni upimaji wa maeneo kwa kuzingatia mpango uliotayarishwa;

**Hatua ya kumi na mbili** ni kutangazwa kwa viwanja vilivyopimwa, kupokea maombi ya wahitaji wa viwanja na ugawaji kwa waombaji waliokubaliwa na kamati ya kugawa ardhi.[20]

**Changamoto:** Kuna changamoto kadhaa zinazokabili ukuaji wa miji nchini, changamoto hizi ni pamoja na kutokufuatiliwa ipasavyo taratibu zilizoainishwa na Sheria ya Mipango Miji kama zilivyojadiliwa hapo juu.

**Kwanza**, ni kukosekana kwa ushirikishwaji wa wanavijiji kwenye vijiji vilivyoko kwenye mpango wa mipango miji;

**Pili**, kumekuwepo na dhana ya kuwa ukuaji wa vijiji kuwa miji hufanyika kwa lengo la kuongeza thamani ya ardhi ya eneo husika hivyo kuchochea soko la ardhi pamoja na kutoza kodi ya ardhi na majengo;

**Tatu**, ni wanavijiji kutokulipwa fidia za haki na kwa wakati. Wakati mwingine wanavijiji hulipwa fidia hata baada ya miaka kadhaa kupita jambo ambalo ni kinyume na taratibu za ulipwaji wa fidia ambazo zinataka fidia kulipwa kwa wakati;

**Nne**, ni utaratibu wa mipango miji kuondoa shughuli zote ambazo zilikuwa zikifanyika katika ardhi ya Kijiji kama vile kilimo na ufugaji na kupelekea wazalishaji wadogo kushindwa kuendeleza ardhi zao pale vijiji vyao vinapotangazwa kuwa miji.

20 Haki za Ardhi Kwa Wakazi Waishio Katika Maeneo Yanayokuwa Kimji: Mada iliyowasilishwa na Hamza K. Sikamkono Afisa Mipango Miji – Mkuranga kwenye Semina ya HAKIARDHI iliyofanyika 26 Agosti 2011.

**Mapendekezo:**

- Wazalishaji wadogo wanahitaji masuala yafuatayo kuzingatiwa katika ukuaji wa miji;
- Kuruhusu ukuaji wa miji wima na sio mlalo ili kuondoa madhara ya kupanuka kwa miji na kumeza maeneo ya vijiji.
- Kuhakikisha taratibu za upangaji wa miji zinazingatia shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo pia kilimo na ufugaji ili kuwezesha wananchi wa kada zote kuweza kumudu na kuendesha maisha yao mijini.
- Kuhakikisha kuwa uchukuaji wowote wa ardhi kwa ajili ya kufanikisha mahitaji ya ardhi kwa matumizi ya umma unafanyika kwa mfumo ulio wazi na utakaompa mmiliki anayepoteza ardhi yake maslahi yatakayoboresha hali aliyokuwa nayo mwanzo.
- Kuhakikisha kuwa mchakato mzima wa ukuaji wa miji unakuwa shirikishi katika kila hatua na elimu ya kutosha inatolewa kwa makundi yote ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, wanawake, vijana, wazee, walemavu n.k.

## 2.5 UKUAJI WA VIJIJI

**Muktadha:** Kwa muda mrefu dhana ya maendeleo ya vijiji imekuwa ikihusishwa na kuongezeka kwa watu, shughuli na huduma ambapo mwisho wake ni kufikia hatua ya kuwa sehemu ya mji. Nadharia hii imepelekea kupungua kwa ardhi ya vijiji ambavyo hubadilishwa na kuwa sehemu ya miji hivyo kubadili pia mfumo wa umiliki na aina ya shughuli zinazopaswa kufanyika katika maeneo ya mji.

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(2) na jedwali la 5 kwenye Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 kinaainisha kuwa kijiji ambacho kimeweza kufikia zaidi ya watu elfu kumi, kina kituo cha afya, shule ya sekondari, soko, maduka 20 yaliyosajiliwa, na mahakama ya mwanzo kinapaswa kujumuishwa kuwa sehemu ya mji.

**Changamoto:** Utaratibu huu wa kupandisha ardhi za vijiji kuwa sehemu ya mji sio tu unapunguza ardhi ya kijiji lakini pia una madhara kwa umiliki wa ardhi na shughuli za kawaida zilizokuwa zinatekelezwa kwenye ardhi ya vijiji. Maeneo ya vijiji yanavyopanda hadhi na kuwa miji mfumo wa umiliki hubadilika pia kutoka mfumo wa umiliki kimila ambao hauna ukomo wa muda na tozo za kodi ya ardhi kwenda kwenye mfumo wa umiliki kwa hati ambao una ukomo wa muda wa umiliki na tozo za kodi ya ardhi. Vilevile, mipango miji haizingatii shughuli za asili za matumizi ya ardhi kama vile kilimo na ufugaji badala yake huzingatia zaidi utengaji wa viwanja vya makazi, biashara na maeneo ya matumizi ya umma kama vile shule.

**Mapendekezo:**

- Ili kuweza kuongeza ulinzi wa ardhi ya kijiji ambayo ndio hutegemewa na wazalishaji wadogo ambao ndio sehemu kubwa ya Watanzania nchini, masuala yafuatayo yanapendekezwa;
- Serikali ihakikishe kuwa asilimia 50 ya ardhi yote nchini inaendelea kuwa sehemu ya ardhi ya kijiji na vyovyote vile haitabadilishwa kwa matumizi mengine.
- Nadharia ya maendeleo na ukuaji wa vijiji ijielekeze katika kuboresha huduma na miundombinu iliyopo kijijini bila kulazimu kubadilisha hadhi ya kijiji kuwa mji.
- Vijiji vitambuliwe kuwa vitovu na msingi wa maendeleo kwa kuhakikisha kuwa uwekezaji wa kutosha unafanyika kuwawezesha wazalishaji wadogo kuwa gurudumu la maendeleo nchini.

## 2.6 UPIMAJI WA ARDHI

**Muktadha:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina jukumu la kusimamia na kuwezesha upimaji ardhi na kutayarisha ramani nchi nzima. Sheria ya Upimaji, sura namba 324 ya sheria za nchi inatoa mamlaka ya upimaji ardhi chini ya Idara ya Upimaji na Ramani iliyopo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika ngazi ya Halmashauri, zoezi la upimaji linaratibiwa na Idara ya Ardhi na Maliasili na upimaji wowote utakaofanyika ni lazima uidhinishwe na Idara ya Upimaji na ramani ya Wizara ya Ardhi.

**Changamoto:** Changamoto zinazokabili upimaji wa ardhi ni pamoja na kasi ndogo ya upimaji wa ardhi ukilinganisha na mahitaji ya wananchi hivyo kupelekea uanzishwaji wa makazi holela. Vilevile, yapo matukio ya upimaji ambayo yamesababisha ongezeko la migogoro ya mipaka ya vijiji hii ni kutokana na ushirikishwaji hafifu wa wananchi wakati wa zoezi la upimaji wa mipaka. Pia, kipaumbele kikubwa kwenye upimaji kimewekwa kwenye ardhi ya jumla na hasa kwenye miradi ya viwanja kwa kuwa imekuwa ikitumika kama chanzo cha mapato kutokana na uuzwaji wa viwanja. Hii imesababisha hali ya upimaji wa ardhi za vijijini na hasa suala la utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji kuwa hafifu kwa kuwa haionekani kama chanzo cha mapato huku ikichangia ongezeko la migogoro ya ardhi inayotokana na kukosekana kwa upimaji.

**Mapendekezo:**

- Serikali iwekeze katika upimaji wa ardhi za vijiji ili kupunguza migogoro ya mipaka kati ya vijiji na umiliki wa ardhi kwa mmiliki mmoja mmoja.
- Miradi ya upimaji inayotekelezwa ni sharti izingatie haki za wakazi wa asili kuwa sehemu ya mipango ya upimaji badala ya kulipwa fidia tu na kuondoka au kupewa viwanja vichache.

## 2.7 MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI YA VIJIJI

**Muktadha:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina jukumu la kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake. Katika kufanikisha jukumu hilo Sheria ya Mipango Miji na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini zote za mwaka 2007 zimetoa mamlaka za utekelezaji wa mipango ya ardhi chini ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Jiji, pamoja na Halmashauri za Vijiji. Mamlaka hizo zimekuwa zikiratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya Taifa, Kanda, Wilaya na Vijiji ambapo mamlaka ya juu ya usimamizi ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini.

**Changamoto:** Pamoja na kuwepo kwa mamlaka hizo za upangaji wa ardhi nchini bado kumekuwepo na changamoto ya kasi ndogo ya utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ukilinganisha na mahitaji halisi. Mpaka kufikia sasa takribani vijiji 2000 kati ya vijiji 12,545 vilivyopo nchi nzima ndio vina mipango ya matumizi ya ardhi. Vilevile kumekuwepo na changamoto ya uwepo wa maslahi binafsi kama vile kutenga maeneo ya uwekezaji, misitu, vyanzo vya maji au maeneo ya hifadhi pekee hivyo kupelekea kuwepo kwa mipango ambayo haikidhi mahitaji ya wanavijiij kwa kuwa haizingatii mahitaji yao halisi.

Halikadhalika, asilimia kubwa ya mipango iliyotekelezwa haijafikia hatua ya mwisho ya mipango kina ambayo inaainisha matumizi ya kina ya kila eneo. Hii imesababisha mipango hiyo ya matumizi ya ardhi kutozingatiwa na wanavijiji kwa kuwa hawaoni manufaa ya moja kwa moja katika kuboresha matumizi yao ya ardhi.

### Mapendekezo:

- Serikali iboreshe mfumo wa uratibu wa mipango ya matumizi ya ardhi ili kufanikisha upatikanaji wa taarifa zenye muunganiko kutoka ngazi ya kijiji, wilaya, mkoa na Wizara.
- Serikali iweke juhudi za makusudi kuwezesha vijiji vyote kufanyiwa mipango ya matumizi ya ardhi ili kupima na kuainisha maeneo ya utekelezaji wa shughuli za kilimo na ufugaji zinazotegemewa na wazalishaji wadogo kuendesha maisha yao ya kila siku.
- Serikali ihakikishe kuwa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji unafikia hatua ya mwisho ya kutekeleza mipango kina ili wanavijiji waweze kupata manufaa ya matumizi ya ardhi zao.
- Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iboreshe mchakato wa utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi ili kuwepo na mfumo utakaosaidia kuondoa msukumo wa maslahi binafsi ya wadau katika kufadhili mipango ya matumizi ya ardhi za vijiji nchini.

## 2.8 UWEKEZAJI KATIKA ARDHI

**Muktadha:** Katika miaka ya 2000, serikali ya Tanzania ilichukua mrengo wa kutazama uwekezaji katika kilimo cha mashamba makubwa. Mtazamo huu ulichagizwa zaidi na mabadiliko ya kisera kidunia na kikanda. Katika hatua nyingine mpango kama Kilimo Kwanza mwaka 2009 na uanzishwaji wa ukanda wa kusini wa kilimo Tanzania (SAGCOT) ilikuwa miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na serikali[21] katika kukuza uwekezaji nchini. Uwekezaji katika ardhi ya vijiji huchukua mashamba makubwa mchakato ambao hujumuisha ulipaji wa fidia na uhawilishaji wa ardhi kwani mara nyingi wawekezaji hawa hutoka nje ya nchi.

Katika mchakato wa upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji wazalishaji wadogo huhusishwa katika mijadala kupitia Mikutano Mikuu ya Vijiji yenye lengo la kupata ridhaa yao. Katika michakato hiyo kumekuwepo na mazingira ya rushwa na utaalamu wa hali ya juu unaowafanya wazalishaji wadogo kutokufikia maamuzi sahihi.

**Changamoto:** Kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazotokana na uwekezaji mkubwa katika ardhi za vijiji ambazo kwa kiasi kikubwa huwaathiri wazalishaji wadogo. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo;

- *Migogoro na wananchi*; Katika maeneo mengi yaliyo na uwekezaji wa mashamba makubwa, kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara baina ya wazalishaji wadogo na wawekezaji. Hii ni mara tu wazalishaji wadogo wanapobaini kuwa kuchukuliwa kwa ardhi yao kuliwaondolea mamlaka ya kulifanyia maamuzi na pia fidia zilizotolewa haziendani na uhalisia wa thamani ya ardhi iliyochukuliwa.

21 Sulle, E. and Nelson, F. (2013); Biofuels Investment and Community Land Tenure in Tanzania , tazama - https://media.africaportal.org/documents/FAC_Working_Paper_073.pdf

- *Uchukuaji maeneo makubwa kuliko uwezo wa kuyahudumia*; Wawekezaji wengi katika maeneo mengi nchini wamekuwa wakichukua ardhi kubwa na kutumia sehemu ndogo tu ya ardhi. Wakati mwingine hutumia ardhi hiyo katika kupata mikopo na kutumia kwa matumizi mengine yasiyoendana na uwekezaji.
- *Kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathimini*; Kutokana na kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kumesababisha maeneo mengi ya uwekezaji kutokuendelezwa kwa muda mrefu hivyo kuwaathiri wananchi ambao ni wahitaji wa ardhi vijijini.
- *Mtazamo potofu wa dhana ya uwekezaji*; Mtazamo na mkazo mkubwa wa uwekezaji nchini wakati wote umekuwa ni uwekezaji kutoka nje hasa wa mashamba makubwa. Mtazamo huu umewaweka nje ya mfumo wa uwekezaji wazalishaji wadogo na kutotambulika kwa mchango wao katika kukuza pato la Taifa.

**Mapendekezo:**

- Kuweka sera na sheria zenye mrengo wa kuwekeza rasilimali na uwezeshaji kwa wazalishaji wadogo ambao ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula na biashara.
- Kuruhusu uwekezaji wa ubia. Kwa kuwa uwekezaji unaohusisha uhawilishaji ardhi umekuwa na changamoto nyingi, ni muhimu kubadili mtazamo na kuwaweka wazalishaji wadogo kama wabia na wanufaika wa moja kwa moja wa uwekezaji. Hii italeta tija kwa wazalishaji wadogo na serikali.
- Kuwekwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya maeneo ya uwekezaji kwa lengo la kuhakikisha uwekezaji huo unakuwa na tija kwa wazalishaji wadogo na serikali pamoja na kuongeza uwajibikaji.

- Katika nyakati ambazo itaonekana ni lazima ardhi kuchukuliwa, fidia inayotolewa ijumuishe tathmini za maslahi ya vizazi vilivyopo na vijavyo ili kuleta maendeleo endelevu na kuepusha migogoro ambayo imekuwa ikileta hasara kwa pande zote zinazohusika.
- Kugawa ardhi kulingana na uwezo wa wawekezaji kuyahudumia. Ikiwa ardhi itachukuliwa kwa lengo la kupewa mwekezaji, ni muhimu kuzingatia uwezo wa wawekezaji hao kuihudumia ardhi husika. Vilevile muda unaotolewa kwa ajili ya uwekezaji uzingatie uhalisia wa upatikanaji ardhi na mahitaji ya wazalishaji wadogo.
- Pamoja na sheria kuruhusu vijiji kutoa hati hafifu kwa wawekezaji bado kumekuwepo na changamoto kwa Halmashauri za vijiji kutekeleza utaratibu huu. Ni jukumu la serikali kuvijengea uwezo vijiji kuweza kutoa hati hafifu za kimila kwa wawekezaji[22]
- Wazalishaji wadogo watambulike kama wawekezaji kutokana na mchango wao kwa Taifa.

22 Kifungu cha 32 cha Sheria ya Ardhi ya Kijiji namba 5 ya mwaka 1999

## 2.9 MFUMO WA TAARIFA ZA ARDHI

**Muktadha:** Moja kati ya malengo ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ni kuhakikisha kunakuwepo na mfumo thabiti wa kutunza na kusambaza taarifa za masuala ya ardhi. Sera inabainisha kuwa ni muhimu kuwa na mfumo mzuri wa taarifa ili kufahamu kiasi cha ardhi kinachomilikiwa, malengo ya umiliki, na kiasi cha ardhi kilichobaki kwa matumizi na maendeleo ya baadae. Hadi Sera inatungwa taarifa za masuala ya ardhi zilikuwa hazipatikani kwa urahisi na hazikuwa sehemu moja. Kwa mujibu wa Sera taarifa muhimu za ardhi zinazotakiwa kuonekana na kupatikana ni pamoja na mahali ilipo ardhi hiyo, ukubwa wa eneo, muundo wake, majina na anuani za mmiliki, aina matumizi, kodi ya mwaka na malipo yake.[23]

Katika kutekeleza matakwa ya sera ya kuwa na mfumo thabiti wa taarifa za ardhi sheria mbalimbali zilitungwa zikiwemo Sheria za Ardhi Namba 4 na 5 za Mwaka 1999, Sheria ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi, Sheria ya Mipango Miji, Sheria ya Umiliki wa Pamoja, Sheria ya Rehani, Sheria ya Upimaji na Tathmini n.k. Utungwaji wa sheria hizi ulikuwa na lengo la kutatua changamoto zinazotokana na mahitaji makubwa ya ardhi lakini zaidi ni kuangalia ongezeko la mauzo ya ardhi ili kuongeza ukusanyaji wa kodi, uhifadhi duni wa kumbukumbu za ardhi na usimamizi na utawala hafifu wa ardhi.[24]

Ili kukabiliana na changamoto tajwa Wizara ya Ardhi toka mwaka 2002 hadi 2016 imefanya mabadiliko katika mifumo ya utunzaji na utoaji taarifa za ardhi kuwa katika mfumo wa kieletroniki kwa kuja na mifumo mikuu mitatu.[25] Mifumo hiyo ni pamoja na mfumo wa ukusanyaji kodi ya ardhi na utambuzi wa wamiliki ardhi (*Land Rent Management System*), Usajili wa upimaji (*survey registration system*), na mfumo wa kitovuti wa kutunza na kusimamia taarifa za ardhi (*Management of Land Information System-MOLIS*). Kwa zaidi ya miaka 15 toka mifumo hii ilipoanza kufanya kazi mwaka 2002 hadi 2018, mifumo hii imekuwa ikifanya kazi bila kutegemeana na hivyo kutoleta muunganiko wenye tija.[26]

23 Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995.
24 Mwaikambo, E & Hagai (2013); The Role of Land Information System in Instigating Development of a National Spatial Data Infrastructure in Tanzania. FIG Working Week. Environmental Sustainability.
25 Bajeti Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2016/17.
26 Bajeti Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2017/18.

Katika kutambua ukosefu wa mfumo unaounganisha kwa pamoja taarifa za ardhi na kuweka kumbukumbu pamoja, mwaka 2019 – 2020 serikali ilikuja na Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System-ILMIS*) na Kujenga Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi. Mfumo huu kwa sasa unatumika katika Manispaa za Jiji la Dar es Salam tu ambapo umepunguza muda wa utoaji wa hati kutoka siku 90 hadi 7 pale ambapo mwombaji atawasilisha taarifa zote zinazotakiwa.

**Changamoto:** Tangu mwaka 2002 mifumo hii ilipoanza kubadilika, malengo ya mifumo hii yamekuwa yakilenga ukusanyaji wa kodi za ardhi zaidi kuliko kuangalia haki za ardhi za wazalishaji wadogo.[27] Pia mifumo hii imekuwa ikiangalia zaidi masuala ya utawala ndani ya watendaji wa serikali kuliko utoaji wa taarifa hizo kwa umma. Changamoto nyingine ni pamoja na mifumo hiyo kuangalia tu sehemu ndogo ya nchi hasa Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Majiji zaidi kuliko kuangalia mfumo wa Kitaifa.[28]

Halikadhalika, mifumo hii imekuwa katika lugha ya Kiingereza ambayo haifahamiki kwa wazalishaji wadogo. Mifumo hii pia imekuwa ikitengenezwa kama sehemu ya kutekeleza miradi ya wafadhili ambayo ina ukomo na inapoisha hukosa uendelezwaji.

**Mapendekezo:**

- Kuweka utaratibu wa kutangaza kila baada ya miezi 6 kupitia vyombo vya habari na tovuti ya serikali taarifa za ardhi hususani kuhusu hali ya usimamizi, umiliki na utatuzi wa migogoro ya ardhi.

27 Wizara ilinunua na kusambaza mashine za kieletroniki (*Point of Sales Machine-PoS*) 238 kwenye ofisi za ardhi zilizoko katika Halmashauri zote nchini na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya.

28 Bajeti Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2020/21.

- Serikali itengeneze mfumo wa kidigitali na unaopatikana kwa kila mtu ukionyesha taarifa zifuatazo; hatua za upatikanaji wa hati, majina ya wamiliki wa ardhi, ukubwa wa ardhi, ardhi ya uwekezaji ilipo na migogoro ya ardhi iliyotatuliwa, n.k.
- Serikali kutenga bajeti ya kutosha katika eneo la taarifa za ardhi ili kutotegemea miradi ya ufadhili inayobadilika kutokana na mahitaji ya wafadhili.
- Mifumo ya taarifa za ardhi zote ziwe katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

## 2.10 MFUMO WA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

**Muktadha:** Migogoro ya ardhi inasababishwa na umiliki na matumizi ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Migogoro hii inaweza kuwa baina ya wazalishaji wadogo, migogoro ya mipaka ya vijiji na vijiji, hifadhi za wanyamapori na vijiji, wananchi na wawekezaji, migogoro ya wananchi na mamlaka za kiserikali n.k.

Mifumo ya utatuzi wa migogoro huanzia katika ngazi ya kijiji ambapo kuna Baraza la Ardhi la Kijiji, Baraza la Kata katika ngazi ya kata, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika ngazi ya wilaya, kanda au mkoa, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani katika ngazi ya kitaifa.

Pamoja na uwepo wa mfumo huu bado kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi. Mfano, katika bajeti ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya 2016/2017 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kinondoni na Temeke pekee kulikuwa na mashauri 3,149 kati ya hayo mashauri 1,692 yalikuwa mashauri mapya.

## Changamoto:

- *Uhaba wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya*; Kati ya Wilaya 139, kumekuwa na Mabaraza 55[29] pekee yanayofanya kazi hivyo kushindwa kuwahudumia wadawa kwa wakati. Hii ni kutokana na kuwa wananchi hulazimika kusafiri umbali mrefu kufuata haki. Pia kutokana na uchache huo, Mabaraza haya yameelemewa na mashauri kiasi cha kushindwa kutoa maamuzi mapema.
- *Rushwa*; mfumo huu wa utoaji haki umekuwa ukilalamikiwa kwa kugubikwa na rushwa na hivyo kusababisha watu kukosa haki kwa wakati.
- *Uwezo mdogo wa wajumbe wa mabaraza ya chini;* Mara nyingi wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji na Baraza la Kata wamekuwa hawawezeshwi katika kufahamu vyema taratibu za utekelezaji wa majukumu yao hivyo kusababisha kupoteza haki za wadawa.
- *Uhaba wa rasilimali fedha;* Mabaraza ya ardhi kwa muda mrefu yamekuwa yakikabiliwa na ukosefu wa rasilimali fedha na hivyo kushindwa kujihudumia na kuchelewesha utoaji haki.
- *Mwingiliano wa kiutawala*; Kwa kuweka mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi chini ya mhimili wa serikali kumevunja misingi ya kikatiba ya utengano wa kiutawala. Jambo hili limesababisha matatizo kwa wajumbe wa Mabaraza kukosa uhuru wa kufanya maamuzi kwa haki ama kuingiliwa na watendaji wa serikali wakati wa kuendesha mashauri. Jambo hili ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia ni kinyume na mapendekezo yaliyowekwa katika Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 iliyopendekeza Wizara ya Ardhi kutojihusisha na utatuzi wa migogoro ya ardhi

29 Hotuba ya Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kuwasilisha bajeti ya mwaka 2019/2020

**Mapendekezo:**

- Ikiwa mfumo wa Mabaraza utaendelea kutumika ni vyema Mabaraza haya yaanzishwe kila wilaya ili kuwakaribia wananchi na kupunguza gharama za kutafuta haki na pia kupunguza mzigo wa Mabaraza katika kupokea na kuamua kesi.
- Ni muhimu kufanya mabadiliko ya mfumo na kuuweka chini ya mfumo mmoja wa kimahakama ili kuondoa mwingiliano wa kimamlaka.
- Inapendekezwa kuweka mifumo ya kushughulika na maadili ya wajumbe na Wenyeviti wa Mabaraza pamoja na mambo mengine ili kuondoa mazingira yanayosababisha utoaji na upokeaji rushwa.
- Kuwekwa kipaumbele katika kuwezesha mabaraza kifedha ili yaweze kujihudumia na kuondoa mianya ya rushwa.
- Kwa mamlaka zinazohusika kuweka mfumo mzuri wa kuwajengea uwezo wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi mara tu wanapochaguliwa na kuthibitishwa.

## 2.11 TATHMINI NA UFUATILIAJI WA MASUALA YA ARDHI

**Muktadha:** Mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa masuala ya ardhi nchini Tanzania haujawekwa bayana katika Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 wala sheria zake. Ingawa mfumo huu haupo bayana katika sera wala sheria, ni vyema kuangalia kuwa hata sheria na sera hizo ni zao la matokeo ya Tume ya Rais ya masuala ya ardhi iliyoundwa mwanzoni mwa miaka ya 1990 ambayo ilizunguka nchi nzima kuangalia mfumo wa utawala, umiliki na migogoro ya ardhi nchini. Taarifa ya Tume imeangalia kwa kutathmini tulipotoka, tulipo na kupendekeza masuala muhimu katika sekta ya Ardhi. Hivyo ni sahihi kusema kuwa tathmini ya kwanza ya masuala ya ardhi nchini ilifanywa na Tume ya Shivji.

Pamoja na Sera kutokuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ulio bayana katika sekta ya ardhi, kumekuwa na aina mbalimbali za ufuatiliaji na tathmini toka 1995 hadi 2016 kama vile mpango mkakati wa utekelezaji wa sheria za ardhi wa mwaka 2005, uboreshaji wa mfumo wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na usambazaji wa taarifa za ardhi na mapendekezo ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi.[30] Katika ngazi ya kimataifa kumekuwa na mabadiliko katika nyanja za ardhi ambapo jumuiya ya kimataifa imepitisha malengo ya maendeleo endelevu 2030 ambayo yameweka malengo katika masuala ya ardhi na ambayo nchi zote zitatakiwa kutoa taarifa.[31] Hivyo basi, ni muhimu kwa serikali kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kama sehemu muhimu katika utekelezaji wa kazi na miradi mbalimbali katika sekta ya ardhi kama inavyopendekezwa hapa chini;

### Mapendekezo:

- Kuwepo na mfumo wa kudumu wa kuhakikisha kuwa Mikutano Mikuu ya Vijiji inakuwa na ajenda ya kudumu ya ardhi ili kuweza kufuatilia masuala mbalimbali ya ardhi.
- Kuwepo na mawasiliano ya moja kwa moja baina ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu juu ya usimamizi wa ardhi.
- Kuwepo na mikutano ya mara kwa mara katika ngazi ya Taifa inayowaleta wadau wote kwa pamoja katika sekta ya Ardhi ili kujadili na kufuatilia maendeleo katika sekta.
- Itengwe bajeti kutokana na vyanzo vyake vya ndani ili kuhakikisha kuwa mipango ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera na Sheria za Ardhi inafanyika.
- Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya ardhi utengenezwe kwa njia shirikishi ili uweze kuunganisha ngazi zote kuanzia vijijini hadi Taifa.

30 Rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 2016.
31 TALA (2017) Marekebisho ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 2016: Ni kwa Maslahi ya nani?

## HITIMISHO

Kwa ujumla haya ndio madai ya wazalishaji wadogo katika sekta ya ardhi ambayo yakifanyiwa kazi na kutatuliwa ipasavyo yataondoa changamoto zinazokwamisha uzalishaji mali katika kukuza uchumi wao na wa taifa kwa ujumla. Madai haya yanagusa mahitaji ya muda mrefu kuhusu usimamizi wa ardhi, ukuaji wa miji, uendelezaji wa ardhi ya vijiji, haki za ardhi za wanawake na walemavu, uwekezaji katika ardhi za vijiji, mipango ya matumizi ya ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi, upimaji wa ardhi, utoaji wa taarifa na masuala ya ufuatiliaji na tathmini.



ROSA
LUXEMBURG
STIFTUNG

HAKIARDHI
LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

**KWA MAWASILIANO ZAIDI TUMIA ANUANI ZIFUATAZO**
Taasisi ya Utafiti na Utetezi wa Haki za Ardhi –HAKIARDHI
Kitalu Na.236 Block 47 Sinza Mori, S.L.P 75885, Dar es Salaam,
Simu +255 22 2771360/ 0784 646752, Nukushi: +255 22 2771362,
Baruapepe: info@hakiardhi.or.tz, Tovuti: www.hakiardhi.or.tz